OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA/ UJIJI
SHULE YA SEKONDARI WAKULIMA

S.L.P 1003,
**KIGOMA**
**14.12.2020**

**Kumb. Na. WKM/SS/JI/2021**

JINA LA MWANAFUNZI ........................................
S.L.P ..........................................
**KIGOMA**

Ndugu,

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WAKULIMA KWA MWAKA 2021**

**1.0: Utangulizi**

Nitumie fursa hii kukupongeza kwa kufaulu mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi iliyofanyika mwaka 2020 na hivyo kupata bahati ya kuchaguliwa kuendelea na masomo katika ngazi ya Sekondari. Hongera sana. Zingatia kuwa watahiniwa wote waliomaliza elimu ya msingi wangetamani kuendelea na elimu ya sekondari lakini kwa kuwa nafasi ni chache wewe umebahatika kuchaguliwa, itumie nafasi hiyo vizuri.

**2.0: Mahali Shule Ilipo**

Shule ya sekondari **Wakulima** ni miongoni mwa shule za kata zilizopo katika Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Ipo maeneo ya Ujiji katika kata ya **Kagera**. Ni takribani kilometa 10 kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa Kigoma/Ujiji. Ukifika eneo la soko la Kagera, utafuata barabara ya lami hadi mwisho wa barabara hiyo na kukutana na barabara ya vumbi inayoelekea dampo la maji taka. Kabla hujafikia dampo hilo, utaiona shule upande wa kulia.

**3.0: Kufungua Shule**

Kufuatia kalenda ya ufunguzi wa shule kwa mwaka 2019, shule ya sekondari wakulima itafunguliwa tarehe **11.01.2021** siku ya Jumatatu. Hivyo utahitajika kuripoti hapa shuleni kuanzia siku hiyo ya tarehe **11. 01. 2021**. Pamoja na kwamba muda wa kuripoti mwanafunzi wa kidato cha kwanza ni kuanzia tarehe tajwa hapo juu hadi March, ni vema mzazi ahakikishe mtoto anaripoti ndani ya kipindi cha juma moja tu ili kurahisisha walimu kuwafundisha watoto wote kwa wakati mmoja.

**4.0 Sare za Shule**

**4.1. Wavulana**

a. Suruali mbili **Dark Blue** aina ya **"Istem"** ziwe na linda za mbele, isibane na iwe na mifuko mitatu
b. Shati 2 nyeupe zenye mikono mifupi na zisiwe na marembo yoyote
c. Mkanda wa ngozi mweusi wenye chuma kidogo kisicho na marembo yoyote
d. Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visivyo na visigino virefu
e. Soksi nyeusi jozi mbili.

**4.2. Wasichana**

a. Sketi 2 za rangi ya zambarau zenye malinda saizi ya kati na ivuke magoti
b. Shati 2 nyeupe mikono mifupi na zisiwe na marembo yoyote
**c.** Kwa wale wanaovaa hijab, washone sketi ndefu inayofika kwenye viatu na hijabu inayofunika mikono, kitamba cha satini kiwe na rangi nyeupe.
**d.** Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visivyo na visigino virefu
**e.** Soksi nyeupe jozi mbili

**5.0Vifaa vya Taaluma**

- Daftari kubwa (counter book) zisizo pungua 11
- Kalamu za bluu za kutosha
- Msaidie mwanao kupata vitabu vya kumsaidia kwani shule haina vitabu vya kutosheleza wanafunzi wote.
- Kalamu ya penseli kwa ajili ya kucholea michoro mbalimbali

**6.0Vifaa vya Usafi shuleni**

- Kila mtoto wa **kiume** anatakiwa kuja na fyekeo **(kwanja)** moja. Kifaa hiki aje nacho **siku ya kuja kuripoti**
- Kwa upande wa watoto wa **kike**, kila mmoja aje na **ndoo** moja tupu yenye ujazo wa lita 10. Pia kifaa hicho kitapokelewa siku ya kuja **kuripoti shuleni**

**7.0 Mambo ya Msingi Mzazi kuyafahamu na kuyazingatia**

**a.** Shule ni ya kutwa, hivyo msaidie mwanao fedha ya chai kwa kila siku kwani wanafunzi wanaondoka saa 11 jioni kila siku isipokuwa siku ya **Ijumaa** na siku zingine kutokana na sababu kadhaa
**b.** Hakikisha mwanafunzi anapata nauli ya kuja shule kila siku hususani kwa wanafunzi wanaotoka nje ya kata ya Kagera
**c.** Shule haina huduma ya afya, hivyo kama mtoto ataugua akiwa shuleni shule itatoa huduma ya kwanza tu na baadae kuwasiliana na mzazi wake kwa hatua zaidi.
**d.** Hakikisha fomu ya taarifa za hospitali inajazwa kwa usahihi na kama mtoto wako ana tatizo ni vema taarifa ya tatizo la mtoto lifahamike kwa uongozi wa shule maana imekuwa ikijitokeza suala la udanganyifu hususani kuhusu afya ya mwanafunzi.

e. Unapokuja kumsajili, uje na nakala ya cheti chake cha kuzaliwa ili kujua tarehe halisi ya kuzaliwa kwa mwanafunzi na hivyo kuepuka tatizo la kupishana kwa taarifa hususani tarehe ya kuzaliwa ya mwanao

f. Kama mtoto wako ana ugonjwa ambao umethibitishwa na daktari na ambao unahitaji kupewa uangalizi maalum, tafadhali unapomleta mtoto huyo kumwandikisha, uje na nakala ya cheti hicho cha Daktari

**8.0 Sheria na Kanuni muhimu za shule**

a. Kutunza mali za umma
b. Kufika shuleni saa 1:15 asubuhi siku zote za masomo
c. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
d. Kuvaa sare ya shule kwa usahihi wakati wote unapotakiwa
e. Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule
f. Kuwa na heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na wanafunzi wengine
g. Kuepukana na magenge ya watu wahuni yanayoweza kupelekea kufukuzwa shule au kusimamishwa kuendelea na masomo kwa kipindi fulani
h. Kuepukana na tabia za wizi, ushoga, uasherati na makosa yanayofanana na hayo
i. Ni makosa kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki migomo na hivyo kusababisha kukosekana kwa amani shuleni
j. Hauruhusiwi kuwa na simu wakati wote uwapo shuleni
k. Kama umeolewa au umeoa, hauruhusiwi kuendelea na masomo
l. Ni marufuku kudharau bendera ya Taifa

**9.0 Makosa ambayo mwanafunzi akiyafanya mojawapo aweza kusimamishwa au kufukuzwa shule**

a. Wizi
b. Uasherati na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, mirungi nk
e. Kupigana au kupiga wanafunzi wenzake/ mwalimu
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g. Kudharau bendera ya Taifa
h. Kukataa/kugomea adhabu kwa makusudi
i. Kuwa mjamzito
j. Kuoa au kuolewa
k. Kumiliki simu ya mkononi na kuja nayo shuleni
l. Utoro wa siku 90 na zaidi
m. Kutofanya mazoezi ya darasani au mitihani itolewayo darasani

KARIBUNI SANA WAKULIMA SEKONDARI

..................................................

MORIS R. BIYARA
MKUU WA SHULE
0756419547/0621165804



HEADMASTER
WAKULIMA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box
KIGOMA